GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

Mapenzi Yangu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 243 **Safar-R/Awwal** 1446 **AH** **Septemba–** 2024 **Ikha** 1403 **HS** **BEI TSH 800/=**

SEMINA YA NDOA YA KIISLAM

Taarifa fupi juu ya semina ya ndoa iliyofanyika kwa ajili ya Lajna Imaillah Kitonga Dar es salaam tarehe 18/08/2024.

Alhamdulillah kwa fadhili za Allah semina hii

UK. 09



Ndoa

يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوْا رَبَّكُمُ الَّذِيْ خَلَقَكُمْ مِّنْ نَّفْسٍ وَّاحِدَةٍ وَّخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيْرًا وَّنِسَآءً ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ الَّذِيْ تَسَآءَلُوْنَ بِهٖ وَالْاَرْحَامَ ۗ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيْبًا

Enyi watu! mcheni Mola wenu ambaye Amewaumbeni kutoka katika nafsi moja, na Ameumba kutoka katika nafsi ile nafsi yenzie, na kutoka katika nafsi hizo mbili Akaeneza wanaume wengi na wanawake; na Mcheni Yeye bilkhususi kwa kuziheshimu fungamano za kidugu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu.

Katika aya hii, imeelezwa kuwa makusudio ya ndoa ni kupata uchamungu, Masihi Aliyeahidiwa anasema kwamba ikiwa mume na mke watafuata njia ya uchamungu, uhusiano wao utageuka kuwa upendo wa kweli - barua ambayo Masihi Aliyeahdiwa alimwandikia Hazrat Nawab Muhammad Ali Khan juu ya kifo cha mke wake wa kwanza.

Uk.03

Mjue Jinni

Sehemu ya Nne.

دیکھ لو میل و محبت میں
عجب تاثیر ہے۔ اک دل کرتا
ہے جھک کر دوسرے دل کا
شکار

Tazameni kuna athari ya ajabu katika kukutana na kupendana. Moyo mmoja kwa kuinama na kuungana na moyo mwingine

Vile vile, katika sehemu nyingine katika Quran Tukufu, Mwenyezi Mungu anasema

هن لباس لكم و انتم لباس لهن :

Wanawake ni vazi kwenu na nyinyi ni vazi la kwao. Yaani mavazi yanalinda staha na heshima ya mtu pamoja na kujipamba. Vile vile, utu wa mume na mke hukamilishwa na kila mmoja wao. Wote wawili wanapaswa kuwa wazuri kwa kila mmoja. Mfano wa maisha ya Rasulullah (saw) yalikuwa ni picha halisi ya kauli hii ya Qur'ani . Wake zake wote wanaonekana kuwa na furaha. Ushirika mzuri wa Rasulullah[saw] pamoja naye ulikuwa wa kiwango cha juu.

Mfano mkubwa wa Hadhrat Khadija[ra] kama mke wake ni mbele yenu kwamba wakati Mtume[saw] alipokuwa akiogopa wakati wa kuteremshwa wahyi kwa mara ya kwanza, Hadhrat Khadijah[as] alitumia nafasi yake ya kupigiwa mfano na akasema wallahi Mwenyezi Mungu hatakupoteza kamwe, wewe ndiwe mtu mkweli, Wewe ni mwenye huruma, Unabeba mzigo wa maskini na wanyonge, wale ambao hawapati chochote kutoka popote, wanalelewa kutoka kwako, Wewe ni mkarimu na unasaidia watu kwenye njia ya haki. Ni kwa njia nzuri alimsaidia mumewe. Hadhrat Khadijah (ra) ni mfano bora kwetu kwamba mume anapokuwa na shida, maumivu au mashaka yoyote, anahitaji

JALSA SALANA, HISTORIA, SHABAHA NA BARAKA ZAKE >UK .05

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Afrika Kimbilio

Historia inaonesha kuumizana badala ya kuungana na kumkabili adui. Mao-Tse-Tung, baba wa taifa la leo la china anasema, ukimfahamu adui umekwisha shinda nusu ya vita.


Tatizo la Afrika ni kutomjua adui. Sio kila anayekuchekea cheko linatoka moyoni. Na huu ni ulimwengu wa mkakati, hila. Jambo lao la kutuangamiza wanalipanga kwa muda mrefu wakati nyinyi mnakoroma. Wanaanza kuwatumia wasanii wao na wasanii wana athari kubwa hususani kwa watoto, wasanii wanasuka nywele. Na kuvaa nguo zisizo na stara. Na vijana hatimae wanasikia wasanii hao wanajihusisha na uchuro wa laana ya mapenzi ya jinsia moja. Tayari mmekwishachelewa. Hatukumkunja samaki angali mbichi sasa tuna kazi kubwa tusikate tamaa, penyenia pananjia.

Kwa mara ya kwanza najivunia hatua za baadhi ya serikali zetu ambazo zimesema kinagaubaga tutakufa na umasikini lakini katu hatuwezi kusaliti mila zetu. Tumefanya makosa mengi toka tupate uhuru, hili naona hasira ni zaidi hata kuliko ile ya kumuondoa mkoloni. Mapenzi ya jinsia moja hapana. Kama mnatuheshimu kama tunavyowaheshimu tusikilize. Si nyinyi katika lugha yenu mna methali Nyama kwa mmoja inaweza kuwa sumu kwa mwingine. Ushoga ni sumu na kila aonjaye sumu hatima yake ni kifo. Dunia sasa itakimbilia tena Afrika kujifunza utamaduni wa kusema hapana kwa ushoga.

Historia inaonesha watu wanapopewa wajibu mkubwa kiwango chao cha kujitolea kinaongezeka hususani kiwango cha uchaMungu.

Dunia kwa hivi sasa inakabiliwa na adui wa kutengenezwa bilkhususi kuimaliza Afrika, madini yetu yanayakodolewa macho. Ardhi yetu yenye rutuba inawatoa udenda. Mapenzi mfungamano wa kijamii vinawakera. Ndio maana usiku na mchana wanatengeneza njama za kugombana sisi kwa sisi na vita vya panzi furaha kwa kunguru! Si kwa manufaa yao sisi tuishi bila kukwaruzana. Na sisi kwa masikitiko makubwa ngoma wanayopiga ndio tunayocheza. Masikini kama senene tumewekwa kwenye mfuko, humo tunaumana na

Nabii Isa[as] wakati akitafutwa na Herode wazazi wake walikimbilia Misri walikopata hifadhi. Mateso yalipozidi Makka Mtukufu Mtume Muhammad[saw] aliwashauri masahaba wahamie uhabeshi. Hivi karibuni Khalifatul Masih wa V Hazrat Mirza Masroor Ahmad[atba] akielezea juu ya hatari ya vita ya 3 ya dunia inayoonesha dalili ya kuikumba dunia amesema ya kwamba Afrika itakuwa katika nafasi nzuri ya kuilisha dunia na kuipa utulivu.



QUR'AN TUKUFU

Surah 5:28-31

28. "Na wasomee habari za watoto wawili wa Adamu kwa kweli, walipotoa sadaka - ikakubaliwa ya mmoja wao na ya mwingine haikukubaliwa. Akasema: Bila shaka nitakuua. (Mwenziwe) akasema: Mwenyezi Mungu Huwapokelea wamchao tu."
29. "Kama utanyoosha mkono wako kwangu kuniua, mimi sitakunyooshea mkono wangu kukuua. Hakika mimi namwogopa Mola wa walimwengu.
30. "Hakika mimi nataka ujibebee dhambi yangu na dhambi yako, na kwa hiyo uwe miongoni mwa watu wa Motoni; na hayo ndiyo malipo ya wadhalimu."
31. "Basi nafsi yake ikamuhimiza kumwua nduguye, ndipo akamwua; na akawa miongoni mwa wenye hasara."

{وَٱتۡلُ عَلَيۡهِمۡ نَبَأَ ٱبۡنَيۡ ءَادَمَ بِٱلۡحَقِّ إِذۡ قَرَّبَا قُرۡبَانٗا فَتُقُبِّلَ مِنۡ أَحَدِهِمَا وَلَمۡ يُتَقَبَّلۡ مِنَ ٱلۡأٓخَرِۖ قَالَ لَأَقۡتُلَنَّكَۖ قَالَ إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ ٱللَّهُ مِنَ ٱلۡمُتَّقِينَ (٢٨) لَئِنۢ بَسَطتَ إِلَيَّ يَدَكَ لِتَقۡتُلَنِي مَآ أَنَا۠ بِبَاسِطٖ يَدِيَ إِلَيۡكَ لِأَقۡتُلَكَۖ إِنِّيٓ أَخَافُ ٱللَّهَ رَبَّ ٱلۡعَٰلَمِينَ (٢٩) إِنِّيٓ أُرِيدُ أَن تَبُوٓأَ بِإِثۡمِي وَإِثۡمِكَ فَتَكُونَ مِنۡ أَصۡحَٰبِ ٱلنَّارِۚ وَذَٰلِكَ جَزَٰٓؤُاْ ٱلظَّٰلِمِينَ (٣٠) فَطَوَّعَتۡ لَهُۥ نَفۡسُهُۥ قَتۡلَ أَخِيهِ فَقَتَلَهُۥ فَأَصۡبَحَ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ (٣١)}

[سُورَةُ المَائِدَةِ: ٢٨-٣١]



NUKUU YA HADITHI

Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] amesema: "Muogope Mwenyezi Mungu popote ulipo, na fuatilia dhambi na wema ili kuifuta, na tenda mema kwa watu kwa tabia njema.

Jami` at-Tirmidhi (Hadith 1987).



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

"Taqwa ni msingi wa maendeleo yote ya kiroho. Ni msingi ambao imani ya mtu inajengwa juu yake. Bila Taqwa, matendo yote ni mila tupu, bila ya kiroho cha kweli. Kiini cha Taqwa kiko katika upendo wa kina na wa kudumu kwa Allah, ambao unaonekana katika kuepuka yote yanayomchukiza Yeye na kujitahidi daima kutenda kulingana na mapenzi Yake. Taqwa ya kweli inahitaji kuwa makini na mawazo, maneno, na matendo ya mtu, na kujitolea kwa dhati kusafisha nafsi kutoka kwa aina zote za uovu."

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

Mjue Jinni

Kutoka Uk 01..

MJUE DAJJALI SEHEMU YA NNE

Enyi waislam jueni kwamba Kwanza tunajifunza kwamba Dajjal angekuwa amejengeka kwa nguvu na angekuwa mweupe mwekundu na nywele zake zingekuwa fupi na zilizopinda. Huu ndio mwonekano wa jumla wa mataifa ya Ulaya leo. Watu wamejengwa kwa nguvu na nywele ni fupi na zilizopinda hadi leo hata wanawake wao wana nywele za namna hiyo. Tuna fahamishwa na hadithi nyingine inayomwelezea Dajjal inasema:

وَحَدَّثَنِي زُهَيْرُ بْنُ حَرْبٍ، حَدَّثَنَا عَفَّانُ، حَدَّثَنَا عَبْدُ الْوَارِثِ، عَنْ شُعَيْبِ بْنِ الْحَبْحَابِ، عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ، قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " الدَّجَّالُ مَمْسُوحُ الْعَيْنِ مَكْتُوبُ بَيْنَ عَيْنَيْهِ كَافِرٌ " . " ثُمَّ تَهَجَّاهَا ك ف ر " يَقْرَؤُهُ كُلُّ مُسْلِمٍ

Hadhrat Anasi bin Malik ana simulia ya kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu[saw] alisema "Dajjal ni kipofu wa jicho moja, na kati ya macho yake pameandikwa neno "K.F.R". ambalo kila Mwislamu angeweza kusoma. [Sahihi Muslim]

Sifa nyingine ambayo tunajifunza kuhusu Dajjal kutokana na Hadith ni kwamba angeandikwa Ka Fa Ra kati ya macho yake na kwamba kila Muumini angeweza kusoma hili. Hii bila shaka ni sifa ya sitiari ya Dajjal. Kwanza, vipi mtu asiyejua kusoma na kuandika anaweza kusoma maneno haya kwenye paji la uso la Dajjal?

Maana ya neno hili ni kwamba Wakristo na mataifa mengine ya Dajjal wangekuwa wanafanya vitendo hivyo vya kutisha kinyume na Uislamu, kwamba mtu yeyote angeweza kutambua uwongo wao kana kwamba umeandikwa kwenye vipaji vya nyuso zao. Mtukufu Mtume[saw] alituambia kwamba Dajjal atakuwa kipofu katika jicho la kulia jambo ambalo linaonyesha kwamba jicho lake la kushoto litakuwa jicho lake lenye nguvu zaidi.

Hii inarejelea hali ya mataifa ya Magharibi ambayo hayana imani na yanafuata tu mambo ya matamanio ya ulimwengu huu. Jicho la kushoto la Dajjal linaelezea mafanikio ambayo Dajjal atakuwa nayo kuhusiana na mali na teknolojia nyingine na harakati za matamanio. Wametangulia kwa njia ambayo haikutarajiwa na mtu yeyote. Kwa mfano, wanasayansi wamekuja na teknolojia zinazowasaidia kupata hazina ya dunia na kuwa na silaha zinazoweza kuharibu dunia nzima. Wameanza kubadilisha uumbaji wa Mwenyezi Mungu kwa vitu kama vile uhandisi wa maumbile na aina nyingine za upasuaji. Yote haya yanaangukia chini ya jicho la kushoto la Dajjal ambalo ni kali sana lakini halimsaidii mtu huyo kwa vyovyote vile.

Imam Raghib amesema: "Na imepokewa kwamba jicho la kulia la Dajjal litakuwa kipofu na hii ina maana kwamba dajjal atakuwa hana sifa za kimaadili zinazosifika, kama elimu [DINI], akili na unyenyekevu".

Tafsiri ya Ahmadiyya ya Dajjal ndiyo tafsiri pekee yenye mantiki na inayowiana kabisa na Qur-aan pamoja na hadith.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s anasema:

"Neno jicho moja halipaswi kuchukuliwa kiuhalisia. Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'ani Tukufu "Na aliye kipofu katika dunia hii basi atakuwa kipofu katika Akhera" (sura ya 17 aya ya 73) Upofu unao elezwa hapa ni dhahiri kuwa maana yake ni upofu wa kiroho na sio wa kimwili. Hivyo katika mjadala unaojadiliwa itamaanisha kwamba Dajjal atakuwa hana uoni wa kiroho, ingawa uoni wake wa kidunia utakuwa mkali na mkubwa sana; na pamoja na hayo, atagundua mbinu za hila zinazosababisha maonyesho hayo ya ajabu, kiasi kwamba atakaribia kuonekana kama mtu anayedai Uungu. hatakuwa na maono ya kiroho hata kidogo, kama ilivyo kwa watu wa Amerika na Ulaya leo ambao wamebobea upande wa kimwili wa maisha hadi ukamilifu" (Izala Auham, Ukurasa 401).

Pia Hazrat Ahmad a.s anasema: "Kuwepo kwa Dajjaliyyat, kinyume na 'Iswiyyat, ni jambo la lazima, kwa sababu kinyume kinaweza tu kutambuliwa kwa kutofautisha.

Vipingamizi hivi vimekuwepo tangu zama za Mtukufu Mtume s.a.w. Alimwita Ibni Swiyyad Dajjal. Na hawa maulamaa, ambao wanapendelea kufuata hadithi kidhahiri tena kwa kutoijali kabisa Qur'ani Tukufu, nayo pia ni matawi ya mti wa Dajjaliyyat. Wanasoma Qur'ani Tukufu lakini hawaielewi.

Kwa ufupi, leo Dajjaliyyat inaeneza mishale yake mingi katika pande zote kama buibui. Kafiri kwa ukafiri wake, mnafiki kwa unafiki wake, mlevi kwa ulevi wake, na maulamaa kwa tabia yao ya kuhubiri bila juhudi ya kuacha uovu wao, wote wanasokota wavu wa Dajjaliyyat. Wavu huu unaweza kubomolewa tu kwa silaha ya mbinguni na kwamba silaha hiyo inaweza kutumika ipasavyo tu na 'Isa ambaye atashuka nayo kutoka mbinguni ni ile ile tu sala na dua." (The Heavenly Sign, Ukurasa 20-21).

Hapo awali Mtume (saw) aliamini kuwa Ibn Swiyyad ni Dajjal, licha ya kuwa hakuwa na neno K.F.R limeandikwa kwenye paji la uso wake, wala hakuwa na jicho lisiloona [kipofu]. Hii inaonyesha zaidi kwamba bishara hizi ni za sitiari. Ni wazi kwamba Mtume (s.a.w) alifundishwa polepole zaidi kuhusu Dajjal na Mwenyezi Mungu mpaka ikafafanuliwa kwamba Dajjal mkubwa si chochote zaidi ya makasisi wa Kikristo.

Mvua ya Dajjal

Sifa nyingine ya Dajjal ni kwamba atakuwa akiiambia mbingu iteremshe mvua na kuiamrisha ardhi kuwahuisha wafu. Kuna ishara zote za sitiari na haziwezi kuchukuliwa kiuhalisia. Tunaona utimilifu wa bishara hii katika nyanja ya kiteknolojia ndani ya mataifa ya Kikristo ya Magharibi. Wamesonga mbele sana kimaendeleo kiasi kwamba inawafanya watu kupoteza imani ya uwepo wa Mwenyezi Mungu kwa vile wamejaribu kuchukua kila jukumu la Mwenyezi Mungu kwa kujifananisha nalo. Kwa mujibu wa Qur'ani Sifa hizi haziwezi kupewa Dajjal kimwili kwa sababu Mwenyezi Mungu Ameweka wazi kwamba hizo ni sifa Zake tu. Mwenyezi Mungu Anasema;

الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَكُمْ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَنْدَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ {23}

Ambaye amekufanyieni ardhi kuwa tandiko, na mbingu kuwa paa, na akateremsha maji kutoka mawinguni, na kwayo akatoa matunda ya kila aina yawe rizki kwenu. Basi msimfanyizie Mwenyezi Mungu washirika na hali nyinyi mnajua (Sura ya 2 Aya ya 23).

Pepo na Moto wa Dajjal vilivyo tajwa na hadithi

Sifa nyingine ambayo amepewa Dajjal ni kwamba atakuwa na Moto na Pepo, na kile kinachoonekana kuwa ni pepo kingekuwa ni Jahannamu, na kile kinachoonekana kuwa ni Jahannam kwa kweli kingekuwa pepo. Bishara hii kuhusiana na Dajjal inaelezea mahubiri ya Dajjal ambayo yanaifanya dini yake kuwa kama Ukristo na sera zake kuonekana kuwa ni ukweli mtupu na kumfanya mtu aonekane kana kwamba watafika mbinguni kwa kumnasibisha Mwenyezi Mungu na mwana, lakini kwa hakika kuwa wanaongoza wenyewe moto. Watu wanaokataa mahubiri yao haya wanafanywa kuonekana kana kwamba watakuwa watu wa motoni, lakini kwa hakika wataongozwa kwenda peponi ikiwa hao watafuata Uislamu na mafundisho yake ipasavyo. Jannah katika Hadith hizi inahusu maisha ya starehe na anasa za kidunia na moto wa Jahannam inahusu kutokuwa na manufaa haya ya kidunia. Inatuonyesha kwamba mtu anayemfuata Dajjal anaweza kuishi maisha ya anasana starehe kubwa lakini anayemkataa Dajjal ataishi maisha mepesi ya Uislamu na hatakuwa na manufaa ya mambo ya kidunia kwa kiwango ambacho Dajjal atakuwa nacho. Pia zinalinganisha mataifa ya Kiislamu na mataifa ya Kikristo. Dajjal hana manufaa ya kiroho.

Hadithi zinasema

UK. 04

Mjue Jinni

Kutoka Uk 03..

kwamba Dajjal atabeba milima ya mkate kwa kijito cha maji. Hii inarejelea tu mataifa ya Magharibi ambayo yanadhibiti ugavi wa chakula wa dunia nzima. Haisambazwi ulimwenguni kote kwa njia yoyote ya haki kama tunavyoona umaskini katika nchi nyingi.

Magharibi ina chakula kingi zaidi kuliko ulimwengu wote ambao unalaza nchi nyingi bila chakula chochote, na kusababisha vifo kila siku. Dajjal hutoa tu wingi wa vifaa hivi magharibi na kuzipuuza nchi zingine.

Punda wa Dajjal

Hadith inayo patikana katika Sahihi Muslim inasema kuhusu usafiri wa Dajjal kuwa: Tukasema [masahaba]: Mtume wa Mwenyezi Mungu, atatembea upesi gani katika ardhi? Hapo Mtume s.a.w akasema: Kama wingu linaloendeshwa na upepo. (Sahih Muslim hadithi namba 2937)

Sasa nini kinaweza kuwa kitu ambacho kina kasi ya haraka kama hivi? Kwa hakika Mtukufu Mtume s.a.w alikuwa aki maanisha ndege. Pia Mtukufu Mtume s.a.w. alisema "Ardhi itaviringishwa kwa ajili yake", ambayo ina maana ya kwamba mwendo wa usafiri wa Dajjal utakuwa wa haraka sana kiasi kwamba ulimwengu ungeonekana kuwa umepungua, kwa sababu ya jinsi mtu anavyoweza kusafiri haraka kutoka sehemu moja ya ulimwengu kwenda kwingine. Pia imeelezwa kwamba "Atalishika wingu kwa mkono wake wa kulia" (Kanzul Ummal, Juzuu ya 7, Hadithi namba 2998).

Hii inahusu mfumo wake wa kupaa juu ya mawingu na Mtukufu Mtume s.a.w pia aliona njozi ambapo alimuona Dajjal akiruka kati ya mbingu na ardhi jambo ambalo linathibitisha zaidi mwendo wake kwa kutumia mafuta kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Hadithi inaendelea kusema "Atalifikia jua katika machweo yake". Katika siku za leo na umri inawezekana kwenda kwa kasi zaidi kuliko harakati inayoonekana ya jua. Pia tunaambiwa "maji bahari yatafikia kifundo cha mguu" ambayo imetimia kikamilifu kwa usafiri wa chini ya maji ikiwa ni pamoja na manowari.

Kuna hadithi nyingi zinazozungumzia punda wa Dajjal. Baadhi ni pamoja na: "Dajjal atajidhihirisha juu ya sura punda mweupe, ambaye masikio yake mawili yatakuwa yametengana yadi sabini (Mishkat Al Dajjal).

"Chini yake kutakuwa na punda mweupe, urefu wa kila masikio yake mawili utakuwa miaka thelathini na baina ya mguu mmoja wa punda wake mwingine utakuwa umbali wa safari ya mchana na usiku" (Kanzul Ummal Juzuu ya 7, Hadith namba 2998).

Jabir bin Abdullah anasimulia. Mtume (s.a.w) alipokuwa akijadili kuhusu Dajjal alisema: Na punda wake ambaye atafikanaye, atakuwa na upana wa mikono 40 kati ya masikio yake mawili. (Musnad Ahmad)

Sasa hakuna Mwislamu anayepaswa kuanza kumngoja punda halisi kwa sababu ya bishara hii. Mtukufu Mtume (s.a.w) alitupa dalili za kutosha ili tuweze kuelewa utimilifu wa bishara hizi. Mtukufu Mtume s.a.w aliweka wazi kwamba huyu hatakuwa punda halisi kwani aliyataja masikio yake kuwa yametengana yadi sabini ambayo hayaonekani ndani ya punda.

Hadith pia inasisitiza kwamba atakuwa mweupe au rangi inayong'aa ambayo pia haipo katika mnyama huyu. Hadithi pia zinaeleza kula kwake moto, ambapo hatuuoni. Maelezo hayo yana maana kamili kwa kuwa ni bishara zinazo elezea kuwepo kwa ndege, treni na magari. Sehemu ambayo imetajwa kuwa hatua moja ingechukua safari ya mchana na usiku inahusu umbali unaoweza kukamilika kwa kutembea kwa kiasi cha saa 24, ni hatua rahisi kwa Dajjal kwa sababu ya usafiri wake kupitia punda huyu. Hii inafafanua zaidi jinsi Dajjal angetumia teknolojia kwa namna ambayo ingemsahau lisha mwanadamu muumba wake wa kweli. Utabiri wa ndege hauko tu katika vitabu vya ahadith vilivyokubaliwa na Waislamu wa Sunni, bali pia katika Vitabu vya Shia kwa undani sana. Kwa mfano hadithi:-

"Angekuwa na vizuizi vya mara kwa mara katika njia yake. Kila kukicha umma ungealikwa kuja na kuketi kabla hajaanza tena safari yake, na kila kuondoka kungetangazwa kwa sauti kubwa" (Biharul Anwar, Babu Alamate zuhuri Alaihis-salam min Al- Sufyani Wa Dajjal)

Angekuwa na vizuizi vya mara kwa mara hii mradi wake ni kwamba kutakuwa na vituo vya ukaguzi ambavyo leo tunaona kuwepo kwa askari wa usalama barabarani lakini pia uwepo wa stendi katikati ya safari za kushusha na kupakia.

Kila kukicha umma ungealikwa kuja na kuketi kabla hajaanza tena safari yake hii mradi wake kutakuwa na matangazo mengi ya ubora wa usafiri huo na njia za kujipatia tiketi na namna bora ya huduma iatakayokuwa ikitolea kwenye usafiri.

Na kila kuondoka kungetangazwa kwa sauti kubwa hapa pia mradi wake ni kwamba katika stendi kubwa za mabasi na ndege kutakuwa na matangazo ya kuwaeleza abiria kuwa muda wa kuondoka umefika na pia tangazo la kuamuru gari au ndege kuondoka endapo muda unapofika kupitia amri ya serikali chini ya Dajjali.

Enyi waislam haya yaliyo elezwa na hadthi kwa uelewa na ufahamu tuliyo nao leo hajatimia mpaka tumsubiri huyo punda mmoja? ambaye kwakweli haitakuja tokea aje.

Kwa kweli nduguzangu kwa uwazi huu uliyo wekwa na Quran na hadithi kuhusu Dajjali bado tuna hangaika na ninini kingine kitakacho tusaidia kumjua Dajjali?

Hii ni faida kubwa kwa waislamu wote kutambua kuwa Imam Mahdi kishafika nayeye ndiye aliye fundishwa na Allah maana hizi za Dajjali.

Kwa mwendelezo wa Makala hii picha simu au WhatsApp +255 658 971 662

Ndoa

ushauri wako zaidi kuliko mwingine wakati huo waungwe mkono kama Hadhrat Khadija alivyofanya. Upendo ulio kwa ajili ya Mungu, starehe ambazo ni kwa ajili ya Mungu, rangi za mapenzi na starehe hizi ni tofauti na starehe zingine za kidunia.

الرجال قوامون Kwa kusema kwamba popote pale ambapo Mwenyezi Mungu ameweka jukumu zito kwa wanaume, amewajibisha wanawake kuwatii waume zao.

Masihi Aliyeahdiwa a.s alisema kwamba ahadi ya Mungu kwa wanawake ni kwamba ikiwa watawatii waume wao, Mungu atawalinda na majanga yote na watoto wao watakuwa na maisha marefu na bahati nzuri. Kuna msemo kwamba nyuma ya kila mwanamume aliyefanikiwa kuna mwanamke. Nini maana ya hii? Hii ina maana kwamba upendo unaostawi ndani ya nyumba humpa mwanamume hali ya usalama na kumsaidia kufanya kazi zake za nje vizuri. Je, mtu anawezaje kutoka na kutimiza wajibu wake katika nyumba ambayo kuna ugomvi wa mara kwa mara?

Kuna hadithi moja ya Mtume (saw): Niliona motoni kuwa kuna wanawake wengi kuliko wanaume. Maswahaba wakasema: Je! wanamkufuru Mwenyezi Mungu? Akasema hapana, wao si watii na hawana shukurani kwa waume zao na hawakubali kukiri kufanyiwa wema. Ukimfanyia mwanamke hisani maisha yako yote na akaona kitu ndani yako ambacho ni kinyume na utashi wake, anasema kuwa sijawahipo kupata kitu kizuri kutoka kwako.

Siku moja Mtume Saw alisema. Mwanamke akifa na mumewe ameridhika naye ataingia Peponi. Katika sehemu nyingine, kuhusu watu watatu, Mtukufu Mtume saw alisema kwamba dua zao hazikubaliwi wala hata amali zao njema hazipandi mbinguni. Miongoni mwa watu hawa katika nambari ya pili ni mwanamke maskini ambaye mumewe amemkasirikia.

Masihi aliyeahidiwa[as] alisema kwamba mume ni mdhihirisho wa Mwenyezi Mungu kwa mke. Imesimuliwa katika hadtihi kwamba Mwenyezi Mungu angeamrisha mtu yeyote kumsujudia min ghairi yake, angemwamrisha mwanamke kumsujudia mumewe.

Kwa mwendelezo wa Makala hii picha simu au WhatsApp +255 658 971 662

JALSA SALANA, HISTORIA, SHABAHA NA BARAKA ZAKE

Na. Wasim Ahmad Khan Sahib, UK

Mtume wetu Mtukufu Seyydna Hadhrat Muhammad Mustafa[saw] alisema ya kwamba hakika kuna baadhi ya malaika watukufu wa Allah wazungukao ili kutafuta mikutano ambamo Allah na Mtume wake hutajwa humo,basi wanapokuta mkutano wa aina hii,huwa wanakaa pamoja nao,na kufunika wenzao kwa mabawa yao na baadaye humweleza Allah hali ya mkutano huo. Washiriki hao wa mikutano hii hupata Baraka nyingi zitokazo kwa Mola wao hata hivyo mwenye kukaa nao bila kutia uzito jambo hilo pia hakosi Baraka zake,bali naye vilevile husamehewa na Allah Karim.

Kwa fadhila na msaada maalum wa Allah,sisi wafuasi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya tumejaaliwa kuwa na mkutano mtakatifu wa aina hiyo ambao hufanyika katika nchi zote ambapo jumuiya ipo na ni sehemu muhimu kati ya mipango inayofanyika kwa mwaka mzima.Tunaweza kuitaja kuwa MKUTANO WA KITAIFA au JALSA SALANA.

Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Syedna Ahmad as alianzisha Jalsa Salana kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na mkutano wa kwanza uliofanyika mnamo mwaka 1891 ulihudhuriwa na wafuasi 75.Syedna Ahmad as akielezea umuhimu wa mkutano huu alisema,mkutano huu msiuchukulie kama mikutano mingine ya dunia bali hili ni jambo ambalo msingi wake umewekwa na Allah naYe Ameyatayarisha mataifa ambayo hivi karibuni yatakuja kuungana nayo. Alisema kwa imani ya hali ya juu na kwa jalali ya kwamba msiyadhani mambo haya hayawezekani,kwa kuwa hiki ni kitendo cha Mweza Yule Ambaye hakuna jambo lisilowezekana mbele yake. Jambo hili la Allah lilitimia barabara na hakuna yeyote aliyeweza kulisitisha hilo.Jumuiya iliendelea kuenea pembezoni mwa dunia na watu wa mataifa mbalimbali waliendelea kuingia katika jumuiya makundi makundi,washiriki wa Jalsa Salana nao waliendelea kuongezeka,hivyo mkutano wa mwisho uliofanyika katika maisha matakatifu ya Syedna Ahmad as mnamo mwaka 1907 watu walioshiriki katika mkutano huo walikuwa 3000.Baada ya kufariki kwa Syedna Ahmad as ukhalifa ulipatikana katika jumuiya na chini ya uongozi huo jumuiya iliendelea kupata maendeleo siku hadi siku na ujumbe wa Islam kwa kupitia jumuiya ulifika duniani kote na pale ambapo ujumbe ulifika na jumuiya kustawi huko nidhamu ya Jalsa Salana ilianzishwa kwa lengo la kuwalea na kuwaelimisha wanajamaati wa nchi husika.Kama nilivyosema kuhusu idadi ya washiriki wa Jalsa,jinsi walivyoongezeka ieleweke ya kuwa mkutano wa mwaka 1983 uliofanyika katika makao makuu ya Jumuiya mjini Rabwah Pakistan,watu wasiopungua Laki Tatu walihudhuria mkutano huo,jambo ambalo liliwatetemesha viongozi wa serekali pamoja na masheikh wa kiislamu akiwemo rais wa nchi Jenerali Muhammad Zia ul Haqq wakawa tayari kuchukua hatua kali dhidi ya Jumuiya na kuimaliza mara moja. Wapinzani hao pamoja na kuchukua hatua ya kupiga marufuku juu ya mkutano wa jumuiya walitengeneza njama ya kuuangamiza ukhalifa lakini LINALOPANGWA NA ALLAH BILA SHAKA YOYOTE KUTIMIA NI WAJIBU,siku nyingi kabla ya kupigwa marufuku juu ya mkutano wa Jumuiya nchini Pakistani mti huu mtakatifu wa Jalsa Salana ulikuwa umekwishapandwa katika nchi mbali mbali duniani na mizizi yake ilikuwa imekwishastawi imara mno.Upande mmoja Jalsa Salana ilianzishwa huko Indoneshiya na upande mwingine msingi wake uliwekwa huko Ghana,mkutano ulipofanywa Marekani basi nchini Uingireza na Ujerumani mikutano ya aina hii ilianza kufanyika na hali ya sasa ndiyo hii ya kwamba kwa fadhila na msaada maalum wa Allah katika maeneo ya mashariki na magharibi,kusini na kaskazini ilmuradi katika sehemu mbalimbali ya dunia mpango wa Jalsa Salana umekuwa sehemu maalum ya kalenda ya Jumuiya na jambo lisemwalo na Masihi na Mahdi wa Mtume Muhammad saw linatimia kwa shani yake pekee,ya kuwa kila taifa litakunywa maji toka chemchem hii.Licha ya kuwa na rangi na makabila tofauti mataifa mbalimbali ya dunia yanaendelea kujifaidisha na silsila hiyo. Jalsa Salana,iwe ikifanyika katika bara yoyote ya dunia ina rangi moja na shani yake isiyokuwa na kifani,na washiriki wa Jalsa hiyo hupata Baraka nyingi zilizomo pamoja na sehemu ya kutosha ya maombi yaliyofanywa na Syedna Ahmad as kwa ajili wa washiriki hao wote.

Syedna Ahmad as kwa kuelezea shabaha ya kuanzishwa kwa Jalsa Salana alisema yakuwa katika mkutano huu elimu na mawaidha mbalimbali yatatolewa ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuendeleza na kuongeza imani,yakini na maarifa,pia watakaoshiriki wataombewa dua maalum mbele ya Allah ili Allah Awakubali hao na kuwapa mabadaliko matakatifu katika maisha yao vilevile faida nyingine ipatakanayo ndiyo hii ya kuwa kila mwaka ndugu wapya watakaojiunga na jumuiya hiyo,kwa kuhudhuria mkutano huo wataweza kukutana na ndugu zao wa zamani na kwa kufanya hivyo mahusiano ya udugu na mapenzi yataongezeka na ndugu atakayetangulia mbele ya haki katika muda huu ataombewa dua maalum katika mkutano huu na kwa lengo la kuwaunganisha ndugu wote wa kiroho na kuondoa ugeni na unafikii kati yao itafanywa juhudi maalum na wale ambao wana uwezo mdogo wa kiuchumi inawapasa kuwa na mpango wa kuhudhuria Jalsa Hii na endapo kwa kufanya mpango na kutumia busara wataanza kuweka akiba kwa ajili ya matumizi ya Jalsa kila siku au kila mwezi na kuweka pembeni basi bila kuwa na shida yoyote watawezakuwa na matumizi ya safari ya Jalsa.

Ndugu wasomaji Jalsa Salana ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ni ushahidi wa kweli wa jumuiya na ni kioo kinachonesha shani ya jumuiya na wanajumuiya kwa jumla.Ingawaje jalsa salana ya jumuiya ya waislamu wa ahmadiyya Pakistan ilipigwa marufuku mwaka 1984 lakini mwaka huo huo Hadhrat Khalifa tul Masihi wa nne ra alihamia Uingireza na mwaka 1985 mkutano uliofanyika huko Uingireza ulipata sura ya mkutano wa kimataifa kwa sababu ya uwepo wa Ukhalifa nchini humo,ni mkutano ambao una umuhimu wake pekee kwani Khalifa Mtukufu wetu anashiriki na kutoa hutuba mbalimbali na kila mwaka mkutano huo unapata maendeleo makubwa katika pande zote pamoja na hayo Khalifa Mtukufu anapanga safari kwenda nchi tofauti na kushiriki katika mikutano yao na pale ambapo Khalifa Mtukufu anakwenda kushiriki mkutanoni,wanajumuiya wa huko wanabahatishwa kumwona Khalifa Mtukufu mbele yao.Tanzania ilibahatika kupokea Khalifa wa Allah mara mbili,mnamo mwaka 1988 alipokuja Khalifa Mtukufu wa nne ra na mnamo mwaka 2005 alipotutembelea Hadhrat Khalifa tul Masih wa Tano Allah Amsaidie kwa msaada Wake maalum.

Jalsa Salana ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ina shani yake isiyopatikana duniani kote katika mikutano ya kidunia,hii ndiyo Jalsa ambayo upande mmoja inadhihirisha ukweli wa Hadhrat Masih na Mahdi as kama asemavyo kuwa,Allah Ameyatayarisha mataifa ambayo hivi karibuni yatakuja kuungana na jumuiya hiyo na upande mwingine inatupa nafasi ya kujiimarisha kiimani,tunapoangalia wapendwa wafuasi wa Jumuiya hiyo ambao huwa tayari kujitolea muda wao na mali yao ili waweze kushiriki mkutano huu na umaskini hauwezi kuwa kikwazo katika njia yao,hii inanikumbusha wanajumuiya wenzangu wa nchi moja ya bara la Afrika Magharibi iitwayo Burkina Faso ambao walipopata taarifa ya kuwa Khalifa wa Allah anatarajia kushiriki katika mkutano wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya utakaofayinka mjini Accra nchini Ghana mwaka 2008 basi mara moja wakawa tayari kushiriki katika mkutano huu,wengine walisafiri kwa njia ya mabasi na malori lakini pamoja na hao walikwepo wapendwa wa Masihi wa Muhammad saw amabo walipanga mpango wa kushiriki katika mkutano huu kwa kutumia baiskeli zao,ndugu wapendwa hao ndio wafuasi wa Jumuiya hii ya Allah,taaria hii iliposhamiri hapa na pale baadhi ya waandishi wa habari walifika kushuhudia mandhari haya na kurekodi katika jicho la kamera zao wakiwa na wasiwasi nyingi moyoni mwao ya kuwa,je hao watu wataweza kumaliza safari yao toka Wagadugu Burkina Faso hadi Accra Ghana ilhali baiskeli zao ni mbovu na zingene zinaonekana zikishachoka tayari lakini hao waandishi wa habari walikuwa wakiona sura yao ya kidhahiri na kama wangeweza kuona hali na jazba na imani yao wasingekuwa na wasiwasi hizi. Ujumbe huu ulitoka huko na kufika salama nchini Ghana na kushiriki katika mkutano na kwa kumwona Khalifa Mtukufu mbele ya macho yao wakamaliza kiu yao ilhali machozi yalikuwa yakitirika machoni mwao.Upande mwingine hao waandishi wa habari waliojumuika huko Wagadugu kwa lengo la kuwasindikiza wafuasi hao wa jumuiya,siku ya pili asubuhi waliweka habari hii katika magazeti yao ikiwa na kichwa cha habari BAISKELI MBOVU LAKINI IMANI MADHUBUTI.

Katika mkutano huu watu zaidi ya laki moja walishiriki,wengine walitokea nchi za jirani wakiwa wamepanda mabasi na malori na wengine walisafiri wakipanda juu ya paa la mabasi,licha ya kuwa na barabara mbovu,vumbi kali na njia ndefu walipofika,hao wapendwa kwenye uwanja wa Jalsa,walikuwa na bashasha ya hali ya juu usoni mwao,miongoni mwa hao walikwepo wakulima ambao walianza kujiandaa siku nyingi kabla ili waweze kushiriki katika Jalsa salana na walipolima mashamba yao,wakatenganisha sehemu maalum kwa ajili ya kupata matumizi ya safari kwenda Jalsa,hivyo wakatekeleza agizo la Hadhrat Ahmad as ya kuweka akiba kwa ajili ya matumizi ya Jalsa.

Ndugu wasomaji Syedna Ahmad as amefanya maombi mengi kwa ajili ya washiriki wa Jalsa Salana na sisi tunaposhiriki kwenye mkutano,pamoja na kupata Baraka zingine pia tunapata sehemu ya maombi haya ambayo yanatufungulia milango mingi ya fadhila ya Allah.Hivyo basi ewe mwanajumuiya uliosikia Mwitaji aliyeita kwenye imani ya kwamba Mwaminini Mola wenu kwa hiyo umeamini uje na uhudhurie kwenye Jalsa hii na upate Baraka na fadhila za Allah.Allah Akusaidie na Awe pamoja nawe katika safari yako. ***Aamin.***

Bustani ya Washairi

WOKOVU

Salamu Ndugu zanguni, kwa mola naegemea,
Alhamdu rahmani, nuru kwa kunangazia,
Nimezaliwa kundini, Ahmad memjua,
Vitabuvye darasani, Mengi akanifumbua,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

kuwekwa msalabani, na damu wakamtoa,
Si wokovu tambueni, mungu alishakataa,
Ismaili jangwani, mola alimkataa,
Kwa wahayi Wa ndotoni, kondoo akamtoa,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

kabla kufika mbeleni, akili yako tumia,
Wema Wa hapo zamani, dhambi vipi jizuia?
Kwa mungu kaa tumboni, au kafara jitoa!!
Hayo si ya kitabuni, Musa alotuambia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Wokovu siyo imani, Bali dhambi kukimbia,
Pata okoka dhambini, bada mola mtambua,
Wokovu msalabani, ulaya wameshikia,
Vipi pombe vilabuni, zinaa nako kuua?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Busara zitumieni, waungwana kutambua,
Pombe mzizi dhambini, si matusi si zinaa,
Duniani chunguzeni, wapi iliko zagaa,
Kama si msalabani, wapi palipozidia?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Wokovu kweli ni nini!?, dhambini tao kutoa,
Mwenyezi Mungu yakini, kwa hoja kumtambua,
Kwa dalili akilini, kumuogopa jalia,
Na Upendo Wa moyoni, pekee kumpatia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Naswali kwa wanadini, vipi dhambi waingia,
Hali mnayo imani, ya Mungu wetu rabia!,
Hamumuogopi manani, duniani natulea,
Hamumpendi rabani, pepo alo iandaa,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Swali ninawajibuni, dhambi linaloibua,
Imani siyo yakini, ujinga pasi tambua,
Moyo ulo nayakini, dhambi haiwezi kaa,
Kama kutwa na gizani, pamoja wezi tulia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Mfano tuoneni, kwa ubongo kutambua,
Jiwe lile mkononi, tiba kila maradhia,
Chafwata nini wadhani, kifua takumbatia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Mfano tugeuzeni, huku tukifikiria,
Jiwe liwe mkononi, pasi wewe kutambua,
Kama lile mkononi, ni sumu yenye kuua,
Tabaki nalo wadhani, mbali utalirushia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Umepata somo gani, kama umefikiria,
Kwa asili insaani, vizuri twajivutia,
Vibaya vya hatarini, hatutaki karibia,
Sasa kwanini dhambini, hatutaki kujitoa?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Enyi Ndugu wanadini, hakika yupo jalia,
Tafuta kweli yakini, dhambini hutojitia,
\Utakuwa adhabuni, kila tendo kikosea,
Pakufikia Motoni, waovu wataingia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Akili zitumieni, yakini kuitambua,
Mifano ya duniani, michache kuangalia,
Hutobaki kiburini, hatari kikuingia,
Mifano ya hapa chini, kwa busara angalia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Je tautia motoni, mkono kifurahia?
Mlimani kileleni, chini tajiangushia?
Kwa hiyari kisimani, radhi utajitupia?
Kama si woga kwanini, hatari hutoingia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Je utalala relini, gari moshi La kujia?
Mkono tia kinywani, mwa simba alo na njaa,
Hautotoka chumbani, moto ukikuwakia,
Hutoruka kitandani, nyoka ukimlalia?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Hatari za duniani, kwa woga utajitoa,
Vipi hatari mbinguni, kwanini wakurubia,
Umeikosa yakini, baya dhambi hujajua,
Heri kuwa mautini, si mola kumkosea,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Za juu juu imani, sababu kuangamia,
Adhabu ilo Motoni, wanadhani ni mzaa,
Wadhani wameamini, mola wajamtambua,
Qiyama hawaamini, mola hatotufufua,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Nimefika ukingoni, mwenye akili kajua,
Wokovu hasa ni nini, dhambi utakuokoa,
Mola ya kweli yakini, ndiyo Tiba maradhia,
Taokoka tambueni, peponi mtaingia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Masihi Omary Kisagwa

NDOA

Twakushukuru Rabana, Ulopitisha harusi
Kwa utulivu mwanana, tena pasipo tatasi
Japomambo yamebana, Umeitia wepesi
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Leo siku ya Harusi, sote tunashangilia
Tena bila wasiwasi, ndugu tunafurahia
Kwa baraka za Kudusi, Dua tunawaombea
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Bibikani mwana wangu, Leo umesitirika
Ni binti wa kakangu, Ali Mbambwa msifika.
Umepata mkwe wangu, Kijana wa lako rika
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Ukatulize akili, Ndoa sio masihara
Mumeo ukamjali, na ukawe mke bora
Uwe na njema kauli, hutacharazwa bakora
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Mumeo ukamlee, mnapokua chumbani
Simkere kwa mayowe, ajihisi yu motoni
Kwa mahaba kamkoe, umdembe faraghan
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Ewe Mwanangu kipenzi, wosia nakupatia
Ukufae kwenye Penzi, lisije kukukimbia
Sala ndo kubwa hirizi, usende kupuuzia
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Mkwe wetu wa hidaya , mke tumekupatia
Shafii Bin Inaya, mwema kwenye jumuia
Dini siipige ngwala, mwisho mkaja jutia
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Leo umekua tunda, katika wake mtima
Hanaye mwingine nyonda, twakujulisha mapema
Daima atakupenda, kwa jina lake Karima
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Rabbi Ghafuru Mjenga, kizazi Awajalie
Kije dini kuijenga, haki kiipiganie
Dunia 'sije wazinga, wakanifanya nilie
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Mwisho zangu shukurani, Namshukuru
RahimaKanijalia hisani, nikaweza kuyasema
Pasipo kuboona somi, kinywani sikugunguma
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.Rajabu
Abasi MkietiAl-Wattani _MleziMasjid Ihsan-Tanga 15-OCT -2020

MWANA WA BARAKA

Rabi Ilahi Ghafuru, Jalilu Mola Rabuka
Wallahi nakushukuru, Shukurani kufurika
Kwa Mwana kunidhukuru, wakiume msifika
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil

Mtoto wetu Raahil, uwe Mwana wa baraka
Atakubariki Jalali, Baraka za kumiminika
Hilo naomba taamuli, mimi tena sinashaka
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil.

Mimi na mama Rehema, kheri tunakuombea
Malezi yalomema, sote tutakupatia
Ya dini yake Karima, Pamoya na ya dunia
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil

Mola akuhifadhi, katika hii dunia
Akukinge na maradhi, ili uweze kukua
Uje dini uikidhi, kwa heshima na Takua.
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil

Jamati yake raufu, uishike tena sana
Naye Masihi mtukufu, kwetu ndio sayidina
Khalifa wetu Ashirafu, Amir ul Muminina
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil.

Nusrati mke wangu, hongera tena hongera
Mama wa watoto wangu, kuzaa ni jambo bora
Pole kwa yote machungu, utaipata sitara
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil

Mimi babayo Rajabu, bado ningali kijana
Na Abasi ndio babu, katawafu mwaka jana
Muombea kwa Habibu, ghofira mola rabana
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil.

Wakatabahu kwaheri,uyashike nilosema
Ukidharau hatari, hapa mwisho na simama
Nakuombe mazuri, kwa mpaji Mola karima
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil.
Rajabu Abasi Mkieti
Al-Wattani -_MleziMasjid Ihsan- Tanga

Ewe muumba mwenyezi, kwa huruma ninalia
Msaada wako mpenzi, hima nausubiria
Nyonge kama sisimizi, nakutafuta kwa nia
Usiniache mpweke, Imani ikapotea

Napojiri kiangazi, Imani isikauke
Isiharibike ngozi, uzuri usitoweke
Nikabaki na majonzi, mbali nawe siniweke
Usiniache mpweke, Imani ikapotea

Uimara wamnazi, nafsi uihimarishe
Vimbunga nazosimanzi, kwazo na unishindishe
Nizitoe nazo Nazi, nikuze nanirefushe
Usiniache mpweke, Imani ikapotea

Masika yakirejea, Kwa maji siangamie
Nichupue nanimee, kama mpunga nikue
Ninywe naniyatumie, wengine wasaidie
Usiniache mpweke, Imani ikapotea

Mwisho nishike kitanzi, shingo langu nitundike
Wadunia upuuzi, niunyonge uondoke
Nibaki nalako penzi, mwilini litawanyike
Usiniache mpweke, Imani ikapotea

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

APUMZIKE INAYA SAHIB

Na Mahmoud Hamsin Mubiru

1964 ni mwaka unaovuta hisia za aina yake katika historia ya nchi yetu. Mapinduzi yalifanyika Zanzibar. Haikupita muda tukapata muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar na kijana wa kiahmadiyya Mohammad Iqbal Dar akalipatia taifa jipya jina Tanzania, mwishoni mwishoni mwa mwaka huo taifa lilipata msiba kwa kumpoteza waziri wa kwanza kufariki wa Tanzania Sheikh Kaluta Amri Abedi na mazishi yake kuongozwa na Maulana Sheikh Inayatullah Ahmad Chaudhry. Na ni mwaka huo huo katika kijiji cha MMEDA, Ahmadiyya maarufu na wa siku nyingi alipojaaliwa na Allah mtoto wa kiume na kumpatia jina la mtawa na mwanachuoni Sheikh Inayatullah. Na ndugu yetu kiongozi wetu ambaye tulimtambua kama Inaya tarehe 06/08/2024 katika Hospitali ya taifa Muhimbili aliitikia wito wa Mola wake na kuaga dunia. Kwa hakika sisi ni wa Allah na kwake tutarejea.

Umati uliohudhuriwa katika mazishi yake yaliyofanyika katika makaburi ya Ahmadiyya yaliyoko Wailesi Temeke tarehe 07/08/2024 na kuhudhuriwa na waahmadiyya na wasiokuwa waahmadiyya ni ushahidi ni kwa jinsi gani alivyojitahidi kuishi kwa wema na mapenzi na binaadamu wenzake. Majirani zake waliguswa sana na kifo hicho na walieleza jinsi alivyoishi nao kwa wema na kila palipohitaji msaada, ushauri hakusita kufanya hivyo. Hakuna mahubiri makubwa kuliko hayo, kuwa alama na shahidi wa hayo unayoyahubiri. Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alitusihi kutoa haki za majirani. Katika hili ndugu yetu alifaulu.

Nao ndugu wa karibu walikuwa na mengi ya kuelezea. Aliwalea. Aliishi nao kwa wema. Aliwasaidia. Maumivu yao yalikuwa maumivu yake. Alijali sana na aliguswa na matatizo ya nduguze na hii ni sawasawa kwani ndugu zenu wa damu wana haki zaidi. Na haki hiyo alijitahidi.

Kwa kiwango kikubwa Inayatullah Seifu Sahib alijitahidi kutimiza haki za Allah na viumbe wake. Isa Munga ambaye yeye anaishi Masjid Salaam anatoa ushahidi kuwa Inaya Sahib hakukosa sala ya jamaa ya Adhuhuri, Alasir, Magharib na Ishaa. Na akifika anakuwa amebeba tabasamu lake usoni na kutoa salaam kwa kila mmoja. Habari tulizozipata



kutoka nyumbani ni kwamba alijitahidi sana katika sala ya Tahajjud na akiwaamsha ahali zake kushiriki katika ibada hiyo.

Kwa hulka njema aliyoonesha alijaaliwa fursa ya kuitumikia Jamati. Alikuwa Sadr Answarullah. Wajibu alioutimiza kwa mafanikio makubwa. Na ametumikia Jamati akiwa mjumbe wa Majlis Amila ya taifa. Katika nyanja zote za uongozi Inaya Sahib alikuwa anapenda kusikiliza na kushauriana. Hulka hizi mbili zilifanya apendwe na kuheshimiwa.

Inaya Sahib alipenda sana kujiongezea elimu. Nakumbuka kila nilipotoa kitabu alikuwa miongoni mwa watu wa mwanzo kukinunua na aliweza kunipa mchango wake katika safari zangu za kwenda kwenye utafiti wa historia ya Ahmadiyya Tanzania. Wakati tunashughulika kujenga shule yetu ya kwanza ya Sekondari, Inayatullah Sahib alitupatia msaada wa hali na mali. Alitoa michango yake ya ujenzi na mara kwa mara alituuliza juu ya maendeleo ya ujenzi . Shule ilipofunguliwa tulikuwa na uhaba wa wanafunzi na wachache tuliowapata changamoto ilikuwa katika kulipa ada ya shule. Wazazi wengi hawakuwa tayari "kuwatelekeza" watoto wao katika shule mpya ambayo hawakuwa na uhakika na kiwango chake. Kuna kisa cha mzazi ambaye baadae aliambiwa kwamba alipomleta kijana wake shule ya sekondari Ahmadiyya Kitonga huku nyuma alianza kulia na kuona ya kwamba ameachwa jangwani. Hivi leo huyo kijana hajutii kusoma shule ya sekondari Ahmadiyya kitonga. Inaya Sahib toka mwanzoni hakuwa na wasiwasi na shule yetu. Yeye alisema mwanangu Shafi haendi popote isipokuwa shule yetu. Katika msimamo huo alikuwepo pia Azizi Ngamilo aliyemleta kijana wake. Inaya Sahib alimleta kijana wake na akawa anatoa ada bila kukosa na hivyo kurahisisha uendeshaji wa shule. Bila ya imani iliyothabiti juu ya uwezo wetu wa kujenga na kuendesha Sekondari kazi hii ingelikuwa ngumu. Waliorahisisha ni watu kama Inaya Sahib ambaye alitupa moyo na akatuambia kwa msaada wa Allah tutashinda.

Wanajamati watatu nawakumbuka kwa mapenzi na heshima walisaidia sana katika harakati za ujenzi wa shule ya Sekondari Ahmadiyya Kitonga. Shule ndio ilikua imeanza kuwaandikisha watoto, pale haikuwa kazi rahisi wapo tunaowafahamu walioishia njiani. Lakini Mkuti, Ngamilo na Inayatullah walionesha mfano mzuri.

Bila shaka kwa wale waliokuwa wanamfahamu Inaya Sahib wanalo la kueleza, litakuwa ni jambo zuri kama yote hayo yanaweza kuandikwa kwani hiyo hasa ndio historia ya Ahmadiyya. Jinsi Ahmadiyya ilivyomfanya mtu awe bora zaidi. Tunatarajia kupokea mengi ambayo in shaa Allah tutayachapisha. Mimi ninalo moja sitalisahau.

Kujipaka uturi na kunukia vizuri bilhususi siku ya Ijumaa ni jambo jema na limesisitizwa. Katika ijumaa moja na Inayatullah Sefu hakukosa ijumaa, tulikumbatiana na nikavutiwa na uturi alikuwa ametumia. Sikuweza kujizuia nikamuuliza uturi huu unaitwaje na unapatikana wapi? Aliahidi kuniletea chupa na ganda lake ili nisipate tabu ya kutafuta uturi huo. Ijumaa iliyofuata wakati tunakumbatiana na tulipomaliza kumbe alikuwa na uturi na kunikabidhi na kusema ni zawadi yako. Nilipatwa na bumbuwazi, lakini muda kidogo nikakumbuka na kusema jazakumullah Ahsan Jaza. Tukio hili linaweza kukupa taswira huyo aliyewahi kuwa Sadr Answarullah alikuwa ni mtu mwenye khulka ya aina gani. Kila Ahmadiyya alikuwa ni ndugu yake na alimuonesha mapenzi ya hali ya juu. Unachokipenda wewe umpendee nduguyo ndivyo alivyofanya 'Inaya' alikwenda dukani na kuninunulia uturi na kunipatia. Hakusubirikuombwa.

APUMZIKE INAYA

Kutimia ni lazima, Rabi akisha amua
Kazi yetu kusimama, na mikono kuinua
Mola Amuweke pema, ndugu alotangulia
Twaomba palipo pema, apumzike Inaya

Akupe zake neema, Cheo chako kuinua
Muumba wetu Rahima, twaomba kuyapokea
Kwako ndio twainama, tukisoma zetu dua
Twaomba palipo pema, apumzike Inaya.

PILPILI YA KUSAGA INAYOKAA MUDA MREFU MAHITAJI;

Pili pili,
Kitunguu thoum,
Tangawizi,
Vinegar,
Chumvi,
Limao,
Mafuta ya kupikia na
Embe bichi ukipata (mie nimekosa)

JINSI YA KUTENGENEZA;
1. Osha pilipili zako na uzitoe vimiti, viweke kwenye chujio zitoke maji.
2. Menya vitunguu swaum, tangawizi na maembe kisha kata vipande vidogo vidogo.



3. Chukua brenda, tia pilipili zako, kitunguu thoum na tangawizi na maembe kisha WEKA VINEGAR kiasi na usage, USISAGE NA MAJI.

4. Zikisha sagika vizuri, weka kwenye sufuria na bandika jikoni. Tia limao/ndimu na chumvi nyingi ili ilingane na ndimu kisha koroga.

5. Ikichemka na kuanza kama kukauka tia mafuta na ukoroge then acha dkk 3-5 kisha ipua mimina kwenye bakuli ipoe.

USIACHE IPOE KWENYE SUFURIA UTAHARIBU SUFURIA YAKO ITATOBOKA CZ VINEGAR NA BATI HAVIPATANI.

Ikipoa weka kwenye chombo ulichoandaa kama ni chupa ama chochote na umemaliza.

PILIPILI YAKO ITAKUWA TAYARI KULIWA NA PILIPILI YAKO HII INA UWEZO WA KUKAA MUDA MREFU BILA KUHARIBIKA
Kwa mapishi zaidi karibu kujipatia vitabu mbalimbali vya mapishi soft copy vina recipe mbalimbali za mapishi



Maisha baada ya kifo

atajishughulisha tu na kula na kunywa kama mtu aliyebarikiwa sana au atakuwa na jambo la kufanya?
Jibu ambalo Uislamu unatoa kwa swali hili kwamba vitendo vinaunda uhai na kwamba kumtenganisha mtu na vitendo ni kumnyima uhai. Maisha bila matendo ni mabaya zaidi kuliko kifo. Ikiwa maisha ya kutokuwa na shughuli yangekuwa jambo zuri, watu wanaopenda urahisi wa ulimwengu huu wangezingatiwa kuwa watu bora na wanaovutia zaidi. Lakini mtu ambaye amepata furaha inayotokana na kazi anajua kwamba furaha ya kweli inategemea matendo na maendeleo. Inaweza kuwa vyema kwa mjinga kubaki bila kazi, lakini hakuna mtu mwenye akili timamu angetamani kuwa bila kazi.

Quran Tukufu inasema:
nuru yao itapiga mbio mbele yao na upande wa mikono yao ya kuume; watasema: Mola wetu, Ututimizie nuru yetu, na Utughofirie; hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. (Q.66:v.9).
Hiyo ni kusema, kila muumini ataendelea kusonga mbele na ataona hatua mpya za maendeleo, ambazo atajitahidi na kutamani kuzifikia. Tena, Quran Tukufu inasema, 'Waumini hawatapata uchovu wowote mbinguni,' ambayo inaonyesha kwamba kutakuwa na kazi mbinguni lakini haitasababisha uchovu au uchovu. (Q.15:v.49).
Katika sehemu nyingine, Quran Tukufu inasema:
"Ewe nafsi uliyoridhia na Mimi, na ambaye sina shaka ndani Yangu, rudi kwa Mola wako Mlezi, hali ya kuwa umeridhika Naye, na Yeye amekuridhia. ingia miongoni mwa waja Wangu na uingie mahali palipo chini ya ulinzi Wangu wa moja kwa moja' (yaani, mahali ambapo sifa kamilifu za Mungu zinadhihirika kikamilifu). (Q.89:v.28-30).
Kwa hivyo, ingawa mwanadamu ana kazi aliyopewa katika maisha haya, wakati wa kazi halisi huanza baada ya kifo. Hapo ndipo mwaminio anakuwa mtumishi mkamilifu wa Mungu, kwani hapo ndipo anapopata fursa kamili ya kuzama ndani yake na kudhihirisha kikamilifu sifa za Mungu.
Kwa hivyo kazi ya mwanadamu haitakoma katika maisha baada ya kifo. Kwa upande mwingine, itaongezeka. Mtukufu Mtume (sa) anasema, 'Peponi waumini watafundishwa, kupitia wahyi, namna mpya za utukufu na utakaso wa Mwenyezi Mungu.' Hii haimaanishi kwamba watafundishwa maneno mapya kwa ajili ya kumtukuza Mungu, kwa maana, hili mtu angeweza kufanya peke yake. Ina maana kwamba watafundishwa, kwa njia ya ufunuo, sifa mpya za Mungu zinazohusiana na utakatifu na utukufu Wake, ili waweze kujaribu kuwa maonyesho ya sifa hizo pia.
Inaweza kuulizwa ni sifa gani mpya za Mungu ambazo hazijajulikana tayari? Jibu kwamba mwanadamu anaweza kupata ujuzi mwingi tu kadiri awezavyo kujifunza kupitia hisi zake. Kwa hiyo, ujuzi wetu wa sasa umewekewa mipaka na uwezo wa hisi zetu. Inaweza kuelezewa kuwa kamili tu kwa kurejelea uwezo wa hisi zetu za sasa. Lakini mwanadamu anapopata hisi mpya, ataweza pia kufahamu sifa mpya, na Mungu akiwa hana kikomo, mwanadamu ataendelea kufanya maendeleo katika ujuzi na utambuzi wa Uungu, na sifa mpya zitaendelea kufichuliwa kwake. Atajaribu kutambua na kuzidhihirisha katika nafsi yake mwenyewe. Maarifa mapya yatafungua nyanja mpya za vitendo. Mwanadamu ataendelea kwenye njia ya maendeleo ya milele, na imani yake katika na ujuzi wa nguvu zisizo na kikomo na sifa za Mungu zitaongezeka kila siku.
Kwa ufupi,peponi ni mahali pa vitendo, sawa na ulimwengu huu ulivyo; ingawa, ni zaidi. Katika maisha haya mtu anawajibika kushindwa na kucheleweshwa, lakini katika maisha yajayo hakutakuwa na hatari kama hiyo. Kwa hiyo, kwa habari ya ujuzi wa kiroho na jitihada za ulimwengu huu ni kama shule, ambapo mtu anaweza kufaulu au kushindwa. Lakini maisha yanayofuata yanaweza kulinganishwa na ya mtu anayejihusisha na utafiti wa kisayansi baada ya kuhitimu. Yeye pia, anapaswa kufanya kazi kwa bidii, na huenda, wakati mwingine anafanya kazi kwa bidii zaidi kuliko mwanafunzi wa chuo kikuu, lakini tofauti kati yao kwamba mwanafunzi huwa na hofu ili asifeli, lakini mfanyakazi wa utafiti hana hofu hiyo.
Mazungumzo haya yanaonyesha pia kwamba baraka na shangwe za kweli za pepo zinatokana na maendeleo ya kiroho na si katika kutosheleza tamaa za kimwili. Quran Tukufu inasema kwamba neema kubwa zaidi ya pepo ni radhi za Mwenyezi Mungu, (Q.9:v.72). na furaha kuu, kwa mujibu wa Mtukufu Mtume (sa) itakuwa ni kumuona Mungu.
Kwa ufupi, katika kupata elimu ya kweli na kamilifu, kufanya matendo mema kwa mujibu wa elimu hiyo, na katika kupata ukaribu na kuungana na Mungu kwa njia hizi mbili ipo pepo ya Muislamu. Haiwezekani kupata kitu kikubwa zaidi kuliko hiki.
Nimeweka hapa mafundisho ya Ahmadiyyat kuhusu maswali yote ambayo ni wajibu wa dini kupata mwongozo. Ninaomba wale wanaosoma niliyosema kwa uangalifu watasadikishwa kwamba mafundisho ya Ahmadiyya yangemwezesha kila mtu kutimiza kikamilifu lengo la kuwepo kwake.
Ubora wa pekee wa Uislamu upo katika ukweli kwamba unampeleka mwanadamu kwa Mungu, na hivyo kuhitimisha mijadala na mabishano yote. Kwa nini mwanadamu ameumbwa? Lengo pekee la uumbaji wake kwamba anapaswa kufikia muungano na Mungu. Kwa hivyo, ni dini hiyo pekee inayoweza kuhesabiwa kuwa na uwezo wa kutimiza kusudi la kweli la dini ambalo hutuwezesha kupata muungano na Mungu, na sio zile zinazotafuta kutupendeza kwa maneno tu.

-MWISHO-

SEMINA YA NDOA YA KIISLAM

ilihudhuriwa na lajna 182, kutoka katika matawi ya Mkoa wa Dar es Salaam na mkoa wa Pwani.

Kama ilivyo utaratibu wa shughuli za Jamaat Semina ilianza Kwa usomaji wa Quran tukufu iliyosomwa na Bi. Zuhura Hassan aliyesoma Sura Annisaa fungu la kwanza. Baada ya hapo ilifuatiwa na usomaji wa shairi kutoka kwenye kitabu cha Ndoa ya kiislam linaloitwa "MUONGOZO" lililosomwa na Bi, Twayiba Saidi.

Sadr Lajna alitoa khutba ya kumkaribisha Mgeni rasmi, na katika khutba yake alielezea lengo la kufanya semina hii ni kutokana na kuonelea uhitaji hasa wa malezi kwenye swala hili hususan kwetu sisi wanawake wa kiAhmadiyya. Sadr Lajna alitoa nasaha zake chache na kisha kumkaribisha mgeni Rasmi kwa ajili ya kufungua rasmi kikao cha semina.

Mgeni rasmi alielezea katika kutekeleza ndoa ya kiislam tunapaswa kuishi kwa kufata miongozo kwa kusoma Quran tukufu na tafsiri, Tusome hadithi,Tuangalie mifano na Maisha ya wake wa Mitume pia Maisha ya Mke wa Syyidna Ahmad as, ili kuona wao waliishi vipi na sisi tuweze kuishi kwa kufuata Maisha yao. Kisha mgeni rasmi akaongoza maombi ya kimya kimya na kufungua rasmi kikao cha Semina hiyo.

UCHAMBUZI WA AGENDA

1) MAANA YA NDOA YA KIISLAM, SABABU ZA KUINGIA KWENYE NDOA NA NAMNA YA KUCHAGUA MCHUMBA. BI. ZUHURA IDDI.

Muwasilishaji alichambua maana ya ndoa ya kiislam lakini pia alitoa sababu zinazofanya watu waingie katika ndoa sawa na mafundisho ya Islam ,Kua na Taqwa/Uchamungu,Kupata stara sura ya 2 aya 188, Kujikinga na maradhi ya kimwili na kiroho, Kukuza kizazi.Pia alitupitisha ni namna gani watu wanapaswa kutafuta wenza kwa ajili ya kuendea ndoa zao. Na baada ya uwasilishaji wake ilifuata michango mbali mbali ya Lajna waliohudhuria.

2) WAJIBU WA MUME NA MKE KATIKA NDOA YA KIISLAM. BI. RADHIA IMRANI.

Halikadhalika msemaji wa pili nae alitupitisha katika wajibu wa kila mmoja katika ndoa kwa maana ya mwanamke kwa mwanamume na mwanamume kwa mwanamke. Alielezea kwa kina kwa kuzingatia mafundisho sahihi ya dini Tukufu ya Islam. Na baada ya uwasilishaji wake pia watu kadhaa walitoa michango yao na kuongezea juu ya mada husika.

3) MILA NA TAMADUNI POTOFU KATIKA NDOA. BI. UMMI KALUTA.

Msemaji wa tatu nae alituelezea juu ya mila potofu ambazo jamii inakumbana nazo katika maswala ya ndoa, na namna ambavyo sisi kama wanajamaat hatutakiwi kuzifuata mila hizo kwani sisi tumemkubali masihi. Akatueleza namna ambavyo Islam inatufundisha juu ya ndoa na kwamba mambo mengine ni upuuzi. Mila zilizotajwa hasa ni kama vile kuzuia bwana harusi kuingia ndani kwa mkewe siku ya harusi hadi atoe pesa mlangoni, kulazimisha kuvaa sare hata pasipo uwezo, kufanya sherehe kubwa kupita kiasi na kukalifisha nafsi nk. Na vile vile baada ya kuwasilisha kwake ilipatikana michango mbali mbali.

4) NDOA YA MKE ZAIDI YA MMOJA NA WANAWAKE WALIO HARAMU KUOLEWA. BI. ZANANA OMARI.

Kisha tulielezwa namna ambavyo Quran imeruhusu mwanamume kuoa zaidi ya mke mmoja na namna gani Lajna wanaweza kuishi kwa wema na wake wenzao kwa kufuata misingi ya dini yetu tukufu lakini pia kwa kutazama mifano hai ya wake za Mtume s.a.w. Na vile vile ilipatikana michango mbali mbali kutoka kwa wanasemina.

Baada ya mada hii tulifunga kikao kwa ajili ya sala na chakula na kisha tukarejea kwa ajili ya kumalizia kipindi cha pili.

Kipindi kilianza kwa Usomaji wa Quran tukufu Suratul Hashr imesomwa na Bi Jamila Kunyang'anya. Na shairi la Masihi aliyeahidiwa as lililosomwa na bi Shadya Ungando

5) BARAKA /FAIDA ZITOKANAZO NA NDOA. BI. NAOMI PAULO

Kisha tuliendelea kupata mafunzo juu ya baraka zitokanazo na ndoa na faida zake kwa kuona mifano mbalimbali ya waliopata baraka baada ya kuingia kwenye ndoa lakini pia namna islam inavyozungumzia faida za kuwa kwenye ndoa.

6) CHANGAMOTO ZA NDOA . BI. ZENA NYANGE.

Pia tulipata wasaa wa kujua changamoto mbalimbali zinazozikumba Ndoa nyingi na namna gani tunapaswa kutatua changamoto zetu lakini pia namna ambayo tunapaswa kuziepuka changamoto hizo, na tulielezwa juu ya mambo mbalimbali tunayopaswa kuyafanya sisi kama Lajna kwa kugusiwa mambo kadhaa kutoka katika kitabu cha Domestic Issues. Vile vile tulielezwa sawa na mafundisho ya Islam namna gani waja wema wanatatua changamoto zao kwa kutoa mifano ya Maisha ya Mtukufu Mtume s.a.w na Maisha ya Masihi aliyeahidiwa a.s na makhalifa wake. lakini pia alizungumzia sura 14 aya 8 na sura ya 2 aya ya 154-158.

Na vile vile wanasemina walichangia mawazo yao.

7) TALAKA NA NAMNA YA KUPATANISHA WAGOMBANAO .BI. MWAMINI KAZEMA.

Pia tulielezwa namna ambavyo talaka ni jambo la kumchukiza Allah lakini pia ni namna gani tunatakiwa kuwa wenye kuweka suluhu mbele kabla ya kuendea talaka. Lakini pia tulielezwa ikitokea suluhu imeshindikana ni namna gani mtu anaweza kuachana na mwenzi wake kwa wema na kuvunja ndoa hiyo katika misingi ya dini ya Islam.

8) MIONGOZO MBALIMBALI YA MASIHI ALIEAHIDIWA NA MAHALIFA WAKE JUU YA NDOA. BI RUKHSANA YASMIN MUZAFFAR

Bi Rukhsana Yasmin Muzaffar alielezea juu ya miongozo mbali mbali iliyotolewa na Masihi aliyeahidiwa a.s na makhalifa wake kuhusiana na swala zima la ndoa na namna gani mke anatakiwa kuwa mtii na namna anavyotakiwa kuitunza familia yake. Alitueleza namna ambavyo Bi Amma Jaan aliishi katika ndoa yake kwa misingi bora kabisa na kuwa na sisi tunatakiwa kufuata mfano wake.

HITIMISHO

Sadr Lajna alihitimisha semina hiyo kwa kuzungumzia masharti ya baiat kutoka katika kitabu Safina ya Nuhu kwamba. "Nitatanguliza dini juu ya dunia, Ataacha kiburi na majivuno na kua mnyenyekevu kwa kila mtu na kuwahurumia viumbe wa Allah (s.w)."kisha kumkaribisha tena Bi Rukhsana Yasmin Muzaffar,kwa ajili ya kufunga semina hiyo naye akatuongoza kwa maombi ya kimyakimya.

Lakini pia ilifanyika semina Morogoro ambapo ilihudhuriwa na Sadr Lajna Taifa na Naib Sadr Lajna Taifa,Semina hii ilikua na washiriki 91.Sadr Lajna Alizungumzia juu ya umuhimu wa mwanamke wa kiislam na namna ya kuishi katika familia yake sawa na mafundisho matukufu ya Islam, na akatoa uthibitisho kutoka katika Qur an na maandiko ya Masihi aliyeahidiwa[as] na makhalifa wake. Na vile vile alizungumzia wajibu/ majukum ya mwanamke wa kiahmadiya katika familia na malezi kwa ujumla.

Wassalaam.

ANGUKO LA MTU LIPO KWENYE KILELE CHA MAFANIKIO YAKE

Na.
Sheikh Shaban Othman Shunda



Imesimuliwa na Hadhrat Abu Hurairah[ra] aliyesema Mtume[saw] amesema: Yeyote anayenyenyekea kwa Allah, Allah anamnyanyua (Muslim)

ambao wamenyanyuka na kuendelea kung'ara katika tasnia mbalimbali ni wanyenyekevu kiasi kwamba wanauwezo wa kuongea na kila mtu na kumsikiliza kila mtu, hata hawa wasanii ambao tunawaona ni kana kwamba hawajali lolote ni wanyenyekevu mno kwa watu. Mfano mzuri ni unapokutana nao katika mazingira ambayo yana kamera huwa wanakuwa wa kawaida kuliko yeyote, yeyote aliyevimba mbawa upepo ulimtupilia mbali na kumpoteza. Hivyo basi sio lazima mtu apotee na kushuka katika umaarufu wake kama akiendelea kuwa mnyenyekevu kwa Mungu na viumbe wake.

Katika muktadha huu wengi hupoteza nafasi, mali, na uwezo wao kwa sababu wanamsahau Mungu katika mafanikio yao au katika kilele cha mafanikio wanageuza

mgongo na kutomshirikisha Allah kuwa sehemu ya mafanikio yao kama aya hii isemavyo:

Hakika Tumewajaribu kama Tulivyowajaribu wenye bustani, walipoapa kwamba watayakata (matunda yake) itakapokuwa asubuhi Wala hawakusema, Insha-Allah:. Basi uliizingia (bustani msiba mkubwa utokao kwa Mola wako na hali wao walikuwa wanalala. Kwa hiyo ikawa kama iliyong'olewa. Asubuhi wakaitana,. Ya kwamba nendeni mapema kondeni mwenu ikiwa mnataka kuvuna. Basi walikwenda huku wakinong'onezana,. Wakisema: Leo maskini asiingie humo mwenu kinyume cha utashi wenu. Na wakaondoka mapema asubuhi wakiwa na nguvu zilizojaa. Basi walipoliona wakasema: Bila shaka tumepotea. Bali tumenyimwa. Mbora wao akasema: Je, sikuwaambieni mbona hamumtukuzi (Mwenyezi Mungu)

Bila shaka aya hizo zinaakisi kabisa mafanikio ya mwanadamu katika maisha haya na mwisho wa wale wenye fikira hizi.

Msanii Birdman wa Marekani aliulizwa kuhusu pesa kumbadilisha mtu yeye alijibu kwamba "Pesa isikubadilishe kaka, ibadilishe jinsi unavyoichukulia familia yako na watoto wako na hayo yote, kaa vidole kumi chini (kuwa mnyenyekevu)".

Nikigeukia upande wa ajali, magonjwa au majaribu yoyote ambayo yanampunguza binadamu kasi katika kufanya vitu fulani, au kumpa binadamu likizo au ishara fulani kuwa punguza kasi, lakini sasa kama mtu hataelewa yale yanayomtokea ni ishara kwa ajili ya jambo fulani akaendelea tu na mipango yake ile ile ya kimaisha basi huenda huko mbele ataumia zaidi. Kwani binadamu huwa tunachagua kujifunza kwa upesi katika matukio magumu, hapa kuna kisa kimoja nimekikumbuka, kuna mtu mmoja alikuwa anamlaumu Mungu kwamba kwanini alipendelee embe tunda dogo kuning'inia juu ya muembe na kuliacha tikiti chini na ukubwa wake. Muda haukupita mrefu akapitiwa na usingizi na embe likampiga kichwani ghafla naye akajijibu kuwa kweli sasa lingeniangukia tikiti!. Hivyo basi misiba, ajali, magonjwa na matukio yoyote yale katika maisha huja ili kukutia hofu na kunyenyekeza na kutufanya tufikirie tena jinsi ya kuyaendea maisha.

Na Hatuzipeleki Ishara ila kwa kuhadharisha. (17:60)

Kuna jambo hapo nataka kulikazia kwa kulifafanua mara nyingi Mwenyezi Mungu hutuongelesha kupitia matukio mbali mbali, kama ingekuwa tunauwezo mzuri wa kuelewa ishara mbali mbali ambazo mwenyezi Mungu hututumia ili kutunusuru katika majanga makubwa basi mara nyingi tusinge ishia pabaya, mfano mara nyingi ajali ya gari ama basi utakuta abiria walishaona ishara mbali mbali ikiwemo kumueleza dereva kuhusu mwendo kasi, au gari iliyumba mara ya kwanza kabla ya kupata ajali, au jambo lolote linaloashiria hatari huko mbele, lakini sasa kuto kuchukua maamuzi juu ya jambo fulani ndiko kunatufanya tuishie pabaya.

Nataka nitoe mfano binafsi ambao unamhusu mtu wa karibu, alikuwa ni kijana ambaye Mwenyezi Mungu amemjaalia uwezo mkubwa sana wa kutafuta riziki na alimjaalia sana kwa sababu alikuwa kashaanza kumiliki vitu kadhaa katika maisha ya kijijini, lakini tatizo lake kubwa ilikuwa ni kupenda starehe na muziki, akisikia kigodoro au disko sehemu fulani basi lazima utamkuta huko na wengine wanasema alikuwa na mtindo wa kupenda wasichana, kilichotokea katika safari zake za usiku kwenda kwenye starehe walipata ajali mbaya ambapo waliingia sehemu wakiwa mwendo kasi, yeye na mwenziwe walijeruhiwa vibaya, lakini alipojiuguza akapona mwendo ulikuwa ule ule tena. Safari hii sasa walikuwa wamepakizana mshikaki wa watu watatu walipata ajali mbaya ambayo ilimfanya abadilishiwe mfumo wa upumuaji na kuwekewa mfumo mwingine na miaka kadhaa baadaye kutokana na mfumo ule kuchakaa ulikatikia kwa ndani na ukapelekea kifo chake kwa kukosa hewa. Labda tunaweza sema angelisoma kwenye ajali ya mwanzo yasingali mkuta makubwa.

Hivyo basi Allah akitupa mtihani fulani katika maisha ni sehemu ya kutuambia kuwa badilisha mwendo wako Mimi sifurahii mwendo huu.

Msingi unarudi pale pale kwamba pindi Mwenyezi Mungu anapokupa neema yake, iwe ni ya fedha, umaarufu, afya, hadhi au wadhifa basi anatarajia utautumia kwa manufaa ya binadamu au viumbe wengine, utakuwa mnyenyekevu na hautakuwa hatari kwa wengine. Laasivyo Allah huuliza kuhusu neema:

Kisha kwa hakika mtaulizwa Siku hiyo juu ya neema (mlizopewa) (102:9)

Firaun na watu wake walipewa ishara nyingi mno na Allah kabla ya kuangamizwa kama Quran inavyosema kuwa walipewa ishara tisa lakini walipozivuka hizo basi waliangamizwa na mfano wale ambao waliogopa na kupata hofu na Allah akawaacha ni watu wa kaumu ya nabii Yunusi au Nabii Yonah, hata nabii wao alijua kuwa hawa wataangamizwa na akahama mji kwa huzuni na hasira lakini huku nyuma wakaomba na balaa likatenguka.

Tukiangalia mifano ya watu maarufu ambao walipata ajali mbaya au kushuka katika ufanisi wa kazi zao, vijana tunasema kupotea na baadaye kujipanga upya na kurudi ni nyingi mno ukihesabu kwa makini utaona kila alipovuma mtu alikutwa na janga au msukosuko, hata Msanii Darasa baada ya kutoa wimbo wake maarufu uitwao 'muziki' aliwahi kupata ajali mbaya.

Lakini dawa ni ile ile kwamba unapoona mara moja au mara mbili vitu haviendi au misiba ama kupoteza kunakuzunguka ni vyema kuchukua mapumziko katika kazi unayofanya na kujaribu kujipa na kuanza tena upya, hivyo basi kama unataka kubaki katika kilele chako cha maisha kuchukua mapumziko ni muhimu mno, kwani kuchukua mapumziko kutakupa nafasi ya kusoma maisha kwa jiha mpya.

Imesimuliwa na Hazrat Anas bin Malik: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (sa): "Laleni mchana, kwani Shetani halali mchana." (Tabarani)

Katika simulizi nyingine imesimuliwa kutoka kwake 'Ewe Hanzalah! (fanya wema) katika vipindi na (pumzika katika) vipindi vingine.' (Sahih Muslim)

Hivyo ili kuepusha maangamio fulani ni lazima mtu achukue mapumziko kwani kukataa kuelewa ishara fulani za Allah na kuchukua somo hupelekea maangamio ya Mtu.

Kitu kingine kikubwa cha kujiepusha na maangamio na kushuka katika maisha ni kuwa na shukurani na kuona mafanikio yote ni kutokana na baraka za Mwenyezi Mungu wala sio kwa sababu ya nguvu yoyote uliyo nayo, Masihi na Mahdi wa zama hizi anaeleza jambo hili kwa uweledi sana kuwa.

Masihi Aliyeahidiwa[as] alisema: Kwa hiyo, ni lazima na ni wajibu kwa Muumini kufanya sijda za kushukuru mbele ya Mwenyezi Mungu wakati wowote wanapobarikiwa na mafanikio ambayo Mwenyezi Mungu hakuacha juhudi zao ziende bure. Matokeo ya shukrani hii yatakuwa kwamba mtu ataongezeka katika upendo wake kwa Mungu Mwenyezi na kukua katika imani. Kwa kweli, hii sio yote; watu wa aina hiyo watabarikiwa kwa mafanikio zaidi kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kwamba ikiwa mtu ataonyesha shukrani kwa ajili ya fadhila Zake, Atamwongezea mtu kama huyo fadhila zake; lakini ikiwa mtu hana shukurani kwa neema zake, basi kumbuka kwamba mtu kama huyo atashikwa na adhabu iumizayo." *(Malfuzat Juz. I, Uk. 151-153)*

Kwa mwendelezo wa Makala hii picha simu au WhatsApp +255 658 971 662

Maisha baada ya kifo

Kutoka 12..

ya joto au baridi; au tena anatenda dhambi kupitia hisi yake ya misuli anapojiepusha kufanya mema au kuiacha katikati ikiwa haijakamilika ili kujiokoa na uchovu. Kwa ufupi ni zile hisi saba zinazomfanya mtu kutenda dhambi, na hisia hizo ndizo zinazomwezesha kutenda mema. Kwa hiyo milango saba ya akhera ina maana ya hisi saba ambazo kwazo mwanadamu anatenda dhambi. Ni hisi hizi saba ambazo kwazo ataonja adhabu katika maisha yajayo, kwani kutokana na kuzoea kwake maovu, zile hisi saba za kiroho zinazolingana na zile hisi saba za kimwili zitadhoofika na kuugua, na zitakuwa, kwa sababu ya hali ya ugonjwa, kuhisi adhabu iliyowekwa kwa wakosaji katika maisha yajayo. Kwa hiyo tunaona kwamba aina zote hizi saba za adhabu zimetajwa ndani ya Quran Tukufu.

Kuhusiana na adhabu inayohusiana na mtazamo wa kuona, Quran Tukufu inasema, 'Na laiti waliodhulumu wangalijua watakapoiona adhabu'. (Q.2:v.166).

Hiyo ni kusema, watashuhudiwa matukio ambayo yatawasababishia uchungu. Mtukufu Mtume (sa) anasema kwamba wataona nyoka, nge na mambo mengine ya kutisha.

Kuhusiana na maana ya kusikia Quran Tukufu inasema:

Na utakapo waona kwa mbali, watausikia ukelele wake na mngurumo wake. (Q.25:v13).

Hiyo ni kusema, miale ya moto wa jahannam itanguruma kwa namna ya kutisha ili kwamba kusikia kwa mngurumo huo kutakuwa ni maumivu na hofu.

Kuhusiana na hisia ya kunusa na kuonja, Qur'ani Tukufu inasema: 'Na atanyweshwa maji machafu; atainywa na kwa shida ataweza kuimeza kwa kuchukia. (Q.14:v.17–18).

Kuhusiana na hisia ya kuguswa, Quran Tukufu inasema:

Wataweka vitanda vyao katika Jahannamu, na juu yao vitakuwa vifuniko vya moto. (Q.7:v.42).

Hiyo ni kusema, wataadhibiwa hata kupitia hisia zao za kugusa. Tena, Quran Tukufu inasema:

Na watakapotupwa kwenye nafasi nyembamba wakiwa wamefungwa, basi wataomba maangamio. (Q.25:v.14)

Kuhusiana na adhabu itakayotolewa kupitia maana ya joto, Quran Tukufu inasema, 'Waonje maji ya moto yanayochemka na pia maji baridi sana.' (Q.38:v.58)

Kuhusiana na adhabu inayotolewa kwa maana ya misuli Qurani Tukufu inasema, 'Siku hiyo zitakuwa na nyuso za watu wenye huzuni na uchovu. (Q.88:v.3-4)

Kwa ufupi, Quran Tukufu inaeleza kwa kina adhabu zitakazotolewa kupitia hisia saba. Hii ina maana kwamba hisi saba za kiroho, ambazo zinalingana na hisi saba za kimwili, zitavunjwa, na zitakuwa njia au mifereji ya adhabu. Matumizi mabaya au matumizi mabovu ya hisi ambayo ni neema kutoka kwa Mungu, yatadhoofisha hisia za kiroho na mambo yote yatakuwa chanzo cha maumivu kwao. matumizi sahihi ya kitu hukiimarisha na kuongeza sifa zake. Kwa hiyo tunaona kwamba malipo yaliyoahidiwa kwa wenye haki yanahusu hisia hizi saba pia. Kila hisia, kuwa na afya njema na imara itakuwa chaneli au chanzo cha raha. Je, huoni kuwa nuru ya jua yenye kupendeza na kuburudisha macho na kufurahisha moyo inakuwa ni chanzo cha maumivu na usumbufu kwa mtu mwenye kidonda cha jicho, kiasi kwamba ikiwa jicho halitalindwa kwa haraka mionzi ya jua, inaweza kupoteza kabisa kuona; au mtu huyo anaweza kuzimia? Vile vile, je, huomba sauti tamu na ya kupendeza inayowapendeza wasikiaji wote inamsumbua sana mtu mwenye ugonjwa wa sikio au maumivu ya kichwa, na ile inayowafurahisha watu wengine inakuwa kwake huzuni na isiyovumilika? Tena huomba hisia ya harufu inapodhoofika huchukizwa na harufu nzuri, kiasi kwamba manukato yanasababisha maumivu ya kichwa kwa baadhi ya watu ingawa ni moja ya baraka za Mungu? Tena, je, huomba hisia ya ladha inapoharibika, kitu kitamu huonjeka kichungu, na chumvi huonjeka vibaya? Kila kitu kitamu kinapoteza ladha yake, na huenda, kinakuwa kichefuchefu. Tena, je, huomba hisi ya mtu ya kuguswa inapofadhaika, kitanda laini kinachoweza kustarehesha na kumfurahisha mtu mwingine, kinakuwa kigumu zaidi kwake kuliko jiwe na kinasumbua kama kitanda cha miiba ambacho humfanya agaregare kwa uchungu. ? Tena huomba mtu anapovurugwa hali yake ya joto, ubaridi ule unaowaburudisha wengine hugeuka kuwa moto kwake na huvua nguo zake na kulalamika kwa uchungu kwa hisia inayowaka mwilini mwake? Tena, huomba wakati wa joto, mtu ambaye ana hisia hii nje ya utaratibu huanza kutetemeka kwa baridi na kujifunika kwa mavazi ya joto wakati wengine wanaweza kutumia barafu na wanaweza kujipepea? Vile vile, je, huomba wale ambao fahamu zao za misuli zimedhoofika, wanafikiria kutembea mzigo usiovumilika na kwa wengine ni burudani; watu wa namna hii wanachoka kabla hawajatembea hatua nyingi? Kwa ufupi, matukio haya yote yanashuhudiwa kila siku; ambayo mtu anaweza kuelewa vizuri asili ya akhera. Ni lazima ikumbukwe kwamba kama vile wema una maisha chanya na matumizi mabaya ya uwezo wa kutenda mema huitwa uovu, vivyo hivyo, baraka za Mungu na neema ni chanya, na maumivu na adhabu ni matokeo ya uharibifu ambao mtu anafanya katika nafsi yake. Mtu mmoja alikuja kwa Mtukufu Mtume (sa) na kusema, 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu anasema kwamba Pepo imeenea kati ya ardhi na mbingu. Ikiwa ndivyo, basi, jehanamu iko wapi?' Mtukufu Mtume (sa) akajibu, 'Inapokuwa mchana, usiku uko wapi? Ndivyo ilivyo kwa pepo na Jahannam.' Sasa hii haiwezi kumaanisha kwamba wakati mmoja watu wote watakuwa Jahannam, na wakati mwingine, wote watakuwa peponi, kama vile kuna siku kwa wakati mmoja na usiku kwa mwingine. Ina maana, badala yake, kwamba ingawa usiku unaijia dunia nzima na mchana pia huja juu ya dunia yote, lakini wale walio na jua juu yao, ni mchana, na kwa wengine ni usiku. Vile vile wale ambao watakuwa chini ya upendeleo wa Mungu, watajikuta peponi, na wengine jahannam. Kwa hiyo wale ambao kwa neema ya Mungu watakuwa wamekuza hisi zao saba katika hali ya uzima watafurahia baraka za peponi, laki wale ambao watakuwa wameharibu hisi zao, baraka hizo hizo zitageuka kuwa adhabu. Watu waadilifu watahisi joto zuri na hivyo itawahakikishia faraja yao, lakini waovu watasikia joto la moto uwakao ambao utawaunguza kwa miali yake. Mtu mwema atafurahia baraka za kiroho zinazofanana na maji baridi, lakini maji yanapotolewa kwa mtu mwovu atayapata yakiwa ya moto sana hivi kwamba yataunguza kinywa chake.

Mtukufu Mtume (sa) anasema: 'Kila mtu ana nafasi peponi na motoni; wale wanaokwenda peponi watachukua sio tu nafasi zao wenyewe bali pia mahali ambazo zingekaliwa na wale ambao wako motoni, na wale wanaoenda motoni pia watachukua nafasi ambazo zingekaliwa na wale walio peponi'

Hii pia ina maana kwamba wakazi wa peponi watachukua furaha yote, na wale waliohukumiwa motoni, watachukua adhabu yote. Mtu asipoweza kufaidika na baraka, humwambia yule mwingine, 'Wewe umechukua sehemu yangu pia. Quran Tukufu inasema; 'Hakuna hata mmoja wenu ambaye hatashuka katika Jahannamu.' Kisha ikaongeza: "Basi tutawaokoa wale waliokuwa nao. (Q.19:v.71-72).

Hii inaonyesha kwamba kila mwanadamu ataingia motoni lakini Mungu atawaokoa wenye haki kutokana na maumivu na mateso. Yaani wataingia motoni lakini wakati huo huo watakuwa salama wakiwa humo. Hii inaweza tu kumaanisha kwamba watu waadilifu watageuza kila kitu kuwa chanzo cha baraka na furaha kwao wenyewe kupitia utimamu wa hisi zao. Mtukufu Mtume (sa) anasema, 'Mwenyezi Mungu atamwambia mtu: 'Rukia motoni.' Atakaporuka ndani yake, atapata mahali pa furaha.' Kwa ufupi, mambo hayo yote ambayo mwili wa kiroho utapitia katika ulimwengu ujao yatakuwa ni matokeo ya matumizi sahihi au mabaya ya hisi saba.

Kuna tofauti hii kweli kwamba wakazi wa motoni watafungiwa kwenye sehemu zao, lakini wakaaji wa mbinguni watakuwa huru, kama vile mgonjwa anavyofungiwa kitandani mwake, wakati mtu mwenye afya anatembea kwa uhuru. Kwa maana, motoni ni gereza au hospitali, na mbinguni ni raha. Kuzimu kuna mipaka wakati mbingu haina kikomo. Mkazi wa motoni hataweza kuvuka mipaka yake. Lakini mkaaji wa peponi atakuwa huru kwenda popote apendapo. Kwake yeye nafasi yote itakuwa peponi, hata kama ataingia mahali ambapo wakosefu wanaweza kuteswa na mateso ya motoni, itakuwa kwake kama bustani ya starehe. Kama vile wakaaji wa motoni wangepata mateso na inamhuzunisha mtu kuona mtu mwingine katika mateso, wafungwa wa motoni watafichwa machoni pa watu wa mbingu pazia ili kuona mateso yao yasiwasababishe maumivu yoyote labda ikiwa wao wenyewe wanataka kuwaona.

Wakazi wa peponi hawatajua hali ya mtu mwingine; kila mmoja atakuwa anajitambua tu mwenyewe. Lakini ikiwa Mungu anataka kumpandisha mtu cheo cha juu zaidi, atamjulisha hali ya mtu aliye juu yake. Kisha mtu huyo atatamani cheo cha juu zaidi, na atatimiziwa matakwa yake.

Je! Thawabu na Adhabu Zitakuwa za Milele?

Swali lingine kuhusu maisha ya baada ya kifo ni kama pepo na adhabu ni ya milele. Jibu ambalo Uislamu unatoa kwa swali hili kwamba malipo (pepo) yatakuwa ya milele lakini adhabu haitakuwa ya milele. Quran Tukufu inasema kwamba mwanadamu ameumbwa ili aweze kuwa dhihirisho kamili la sifa za Kimungu. Ikiwa watu wataendelea kuwaka katika moto wa mateso milele na milele, ni jinsi gani, na lini watakuwa maonyesho hayo? Quran Tukufu inatuambia kwamba baraka za mbinguni hazitakuwa na mwisho, lakini hii haitakuwa hivyo kwa adhabu ya Jahannamu ambayo, kwa mapenzi ya Mungu na kwa rehema na neema Zake, hatimaye itafikia kikomo. Quran Tukufu inasema kwamba rehema za Mwenyezi Mungu ni kubwa kuliko ghadhabu yake. Wakati waovu watakuwa wamepitia ghadhabu ya Mungu katika kipindi kirefu cha kutosha kuitwa cha milele kwa mtazamo wa maono yenye mipaka ya mwanadamu, rehema ya Mungu itaanza kutenda. Mtukufu Mtume (sa) anasema, 'Utakuja wakati juu ya Jahannam ambapo hakutakuwa na yeyote ndani yake, na upepo wa mashariki utaitikisa milango yake.' Wazo la kwamba wakazi wa jahannam watapata adhabu ya milele sababu ya kutojua kusudi ambalo Mungu huwaadhibu wenye dhambi. Mwenyezi Mungu, kwa kuwa ni Mwingi wa Rehema, hataki kuadhibu mtu yeyote; mtu hujiletea adhabu kwa sababu ya uovu wake mwenyewe. Mwanadamu anapoharibu uwezo wake wa kiroho, hataweza kupata baraka za Mungu za kutunukiwa katika ulimwengu ujao, na hivyo atapata maumivu. Mungu, kwa rehema zake, ameagiza kwamba magonjwa yapate tiba. Kwa hiyo, kama vile magonjwa ya kimwili yanavyoponywa, vivyo hivyo waovu wataponywa na kurekebishwa na maumivu watakayopata na kisha wataweza kufurahia baraka za mbinguni. Kisha wataingia mbinguni, na rehema ya Mungu itakamilika na kusudi ambalo mwanadamu aliumbwa kwalo litatimizwa.

Je, kutakuwa na Matendo Mbinguni au yatafikia Mwisho?

Swali lingine muhimu bila kujibu ambalo maelezo yoyote ya maisha baada ya kifo lazima yabaki kuwa hayajakamilika ni, mwanadamu atafanya nini katika maisha yajayo? Je, matendo yake yataisha? Je,


Ukurasa 08

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE





APUMZIKE INAYA SAHIB

HABARI UK> 09

Maisha baada ya kifo

Kutoka toleo lililopita.

Kwa hivyo, divai hapa ina maana ya upendo wa Mungu ambao mwanadamu anahisi katika maisha haya na ambao utaonekana kuwilishwa kama divai katika maisha yajayo, kama vile katika ndoto hali za kiroho huonekana kwetu katika sura za kimwili. Kwa vile divai hiyo itakuwa kielelezo cha upendo wa Mungu na haitakuwa kitu cha kimwili, kunywa kwayo kutasafisha nafsi ya mwanadamu ikiongezeka hivyo upendo wake kwa Mungu.

Kwa ufupi, wakati Uislamu unaeleza thawabu na adhabu za maisha yajayo kuwa ni za kimwili, unazibainisha kwa wakati mmoja kama za kiroho; na haya ndiyo maelezo pekee ya kweli na sahihi. Wale wasiojua uhalisi ama wamezichukulia kama hali za kimwili au za kiroho tu. Kwa kweli hali hizi zote mbili zinapingana na akili. Thawabu na adhabu za maisha yajayo haziwezi kuwa za kimwili kabisa, wala mtazamo wa kiroho juu yao hauwezi kuwa mwisho kwa mtazamo, kwa kuwa kitu chenye hila na nyeti kinaweza kudhihirisha sifa zake kupitia mwili usio na hila na mbaya kuliko yenyewe.

Adhabu na Thawabu za Ulimwengu Ujao zitajidhihirisha wapi na kwa namna gani

Inaweza kuulizwa ni wapi na kwa




namna gani adhabu ya akhera itajidhihirisha. Uislamu unatoa jibu zuri kwa swali hili, wakati hakuna dini nyingine inayotoa jibu. Uislamu unatufundisha kuwa jahanamu ni jina la adhabu ambayo mwanadamu ataipata kupitia hisia zake saba. Qur'an Tukufu inasema: 'Jahannamu ina milango saba ambayo kila mmoja atapita sehemu moja ya aliyehukumiwa.' (Q.15:v.45)

Lakini tunaona kwamba Qur'ani Tukufu inawawakilisha wote walioingia peponi na wale wa motoni kama viumbe kamili na sio kama viumbe vilivyogawanyika vipande vipande.

Kwa hiyo kuingia kwa sehemu moja ya mwanadamu kupitia kila mlango wa akhera kunaweza kumaanisha tu kwamba mwanadamu ataihisi adhabu yake kupitia njia za hisia zake saba na hivyo ataingia moto kupitia milango saba na kupitia kila mlango hapo itapita sehemu moja ya mwili wake; yaani, sehemu moja kupitia hisia ya kuona, sehemu nyingine kupitia hisia ya kusikia, tatu kupitia hisia ya kunusa, nne kupitia hisia ya ladha, tano kupitia hisia ya kugusa, sita kupitia hisia ya joto/baridi na saba kupitia hisia ya misuli. njia ya hisia hizi saba mwanadamu anatenda dhambi. Anatenda dhambi ama kwa macho yake, anapotazama mambo maovu kwa jicho baya au anatenda dhambi kupitia masikio yake anaposikiliza porojo au lugha chafu n.k.; au anatenda dhambi kupitia pua yake anaponusa vitu ambavyo hapaswi kuvinusa, au kwa hisia yake ya kuonja anapokula vitu ambavyo hapaswi kuvila; au kupitia hisia yake ya kugusa wakati tamaa ya vitanda laini na matakia inamzuia kujitoa katika huduma ya wanadamu wenzake; au anatenda dhambi kupitia hisia yake ya joto wakati anapopungua kutokana na utendaji wa matendo mema kwa hofu

HABARI UK> 11



Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 2,300/=.

Je, Wajua?

Vivyo hivyo, Jua lina gravity kubwa kuliko dunia, na jua huvuta dunia kuielekea. Kinachofanya dunia isivutwe na kumezwa na jua ni kwa sababu inalizunguka jua kwenye mhimili fulani. Vivyo hivyo, dunia ina gravity kubwa kuliko mwezi na ingeweza kuuvuta mwezi kama mwezi usingekuwa unaizunguka dunia. Satellite pia hazianguki duniani kwa sababu zinaizunguka dunia kwenye mhimili.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com